

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG.



SHULE YA SEKONDARI SUMAYE
S. L. P 60, KATESH
HANANG –MANYARA
14/12/2020

KUMB. NA SSS/J.INS/VOL. 1
Ndg. Mzazi/Mlezi wa

.....
.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA
SEKONDARI SUMAYE MWAKA -2021.**

Ninayo furaha kukutaarifu na kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka wa masomo 2021. Hivyo unatakiwa kuripoti shuleni siku ya Jumatatu tarehe 11/01/2021 saa 1:30 asubuhi.

Tafadhali fika shuleni ukiwa tayari kupokea, kutekeleza, na kutii maagizo na sheria zote za shule bila usumbufu wowote. Ni matumaini yangu kuwa utatumia nafasi hii vizuri kwa kujifunza kwa bidii ndani na nje ya shule.

Mwanafunzi atakayechelewa ndani ya siku saba (7) tangu siku ya kuripoti, atahesabiwa kuwa hataki nafasi aliyopewa hivyo atapewa mwanafunzi mwingine na **MZAZI/MLEZI ATAKAYEACHA KUMLETA MTOTO WAKE SHULENI KWA KISINGIZIO CHOCHOTE KILE ATACHUKULIWA HATUA KALI ZA KISHERIA.**

MAHITAJI KWA MWANAFUNZI

1. VIFAA VYA DARASANI

- A) Madaftari makubwa 12 (COUNTER BOOK QUIRE 2)
- B) Kalamu (bluu/nyeusi), penseli, rula na mathematical set.

2. CHAKULA

- A) Mahindi debe nne (4), maharage debe moja na nusu ($1\frac{1}{2}$) na **Tsh 56,000/-**kwa mwaka. (Unaweza kulipa nusu ya mahitaji kwa muhula)
- B) Sahani moja na bakuli moja za kawaida pamoja na kijiko kimoja.

NB: Kwa wanafunzi wa kike watakao hitaji kukaa hostel, wazazi wao wafanye mawasiliano na uongozi wa shule mapema kuomba nafasi hiyo.

Aidha, mahitaji ya hostel ni kama ifuatavyo;

- i. Mahindi debe nane, maharage debe tatu na **Tsh: 187,800/-**kwa mwaka, ambapo unaweza kulipa nusu kwa muhula.
- ii. Ndoo ndogo mbili, sahani au bakuli mbili, kikombe, na kijiko (spoon).
- iii. Sare za hosteli ni sketi rangi ya kaki, tisheti au flana ya bluu, traksuti nyeusi au bluu, mashuka rangi ya bluu au pink, blanket na chandarua ni muhimu sana kwa sababu kuna mbu wengi. **malipo yote ya fedha yalipwe kupitia akaunti zifuatazo: (a) 41010006291, NMB (Chakula Sumaye Sekondari)**

(b) 41010010246, NMB (Hostel Sumaye Sekondari)

3: SARE ZA SHULE

- A) Suruali mbili (2) kwa wavulana (kitambaa kimeambatanishwa na fomu hii) na mkanda mweusi wa ngozi.
- B) Sketi mbili (2) kwa wasichana, kitambaa kimeambatanishwa na fomu hii.
- C) Shati za rangi ya lait bluu mbili (2) mikono mifupi
- D) Sweta za rangi ya laiti bluu mbili (2)
- E) Soksi kwa wasichana rangi nyeupe (stocking) pea mbili (2) na wavulana soksi za khaki pea mbili (2)
- F) Nguo za michezo-fulana mbili (2) za bluu zisizokuwa na maandishi na bukta mbili (2) za bluu.
- G) Viatu vyeusi kwa wavulana na wasichana vyenye kamba **NA VISIVYO VYA KISIGINO KIREFU, PLASTIKI (BAJAJI) AU BUTI .**

Fomu NA.1, iliyoambatanishwa nyuma lazima ijazwe na Mganga mkuu/Wilaya/Kituo cha Afya au zahanati ya serikali kama inavyo elekeza.

MUHIMU: NI MARUFUKU KUVAA NGUO FUPI NA MLEGEZO KWANI KUFANYA HIVYO NI KUKIUKA MAADILI KWA MAKUSUDI. UKIBAINIKA HATUA KALI ZITACHUKULIWA DHIDI YAKO.

MAWASILIANO; 0784438056/0769438282 -MKUU WA SHULE

; 0683181128 -MAKAMU MKUU WA SHULE.

KARIBU SANA SUMAYE SEKONDARI



KUNDA HK.

MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
SUMAYE SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 50 KATESH